# MKUTANO MKUU WA 22 WA WANAHISA NA TAARIFA YA BENKI KWA MWAKA 2023

“MJASIRIAMALI, MAFANIKIO YAKO NI MAFANIKIO YETU”



## MJASIRIAMALI, MAFANIKIO YAKO NI MAFANIKIO YETU

Usikivu na ubunifu umetuwezesha kuanzisha na kuendelea kuboresha huduma tunazotoa kwa wajasiriamali wenye mahitaji mbalimbali.

Tunathibitisha dhamira yetu ya kutoa huduma kwa wajasiriamali popote pale tulipo Tanzania. Pamoja, tutajenga mustakabali ulio imara, thabiti, na wenye mafanikio, tukiwa tayari kukuunga mkono kufanikisha ndoto na mipango yako.



# YALIYOMO

Kurasa


12 22.2 Kuridhia agenda ya mkutano mkuu wa 22 wa Mwaka

12 22.3 Kuthibitisha kumbukumbu za mkutano mkuu wa 21 wa mwaka

15 22.4 Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka

15 22.5 Kupokea na kuridhia taarifa za Bodi ya Wakurugenzi na hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2023

16 22.5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioshia tarehe 31 Disemba 2023

19 22.5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioshia tarehe 31 Disemba 2023

25 22.5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba 2023

29 22.6 Kupokea na kuidhinisha pendekezo la kuongeza mtaji wa benki kwa njia ya hisa stahiki

30 22.7 Kupokea taarifa ya kuisha kwa muda, kuongeza muda na uteuzi wa wajumbe wa bodi

32 22.8 Kuteua mkaguzi huru wa hesabu za mwaka wa fedha unaoishia 31 Disemba 2024

32 22.9 Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi

32 22.10 Kupanga tarehe ya mkutano mkuu wa mwaka wa 23



# Taarifa za Kampuni

**OFISI ILIYOSAJILIWA**

Jengo la DCB House, Kitalu Na. 182 - R,
Magomeni Mwembechai,
S.L.P 19798,
Dar es Salaam.

**KATIBU WA KAMPUNI**

Ms Regina Mduma,
Jengo la DCB House,
Kitalu Na. 182 - R,
Magomeni Mwembechai,
S.L.P 19798,
Dar es Salaam.

**WAKAGUZI**

PricewaterhouseCoopers,
369 Mtaa wa Toure,
Oysterbay,
S.L.P 45,
Dar es Salaam.

#D63F2A

## VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| AGM | Mkutano Mkuu wa Mwaka |
| ATM | Mashine ya kutoa na kuweka Fedha |
| ALCO | Kamati ya Mali na Dhima |
| BOT | Benki Kuu ya Tanzania |
| CIR | Uwiano wa mapato na matumizi |
| CMSA | Mamlaka ya masoko ya mitaji na Dhamana |
| DCB | Benki ya biashara ya DCB |
| DSE | Soko la Hisa la Dar-es-Salaam |
| EAD | Kadirio la hasara ya mikopo isiyolipika ya benki |
| ECL | Matarajio ya baadaye ya hasara ya mikopo |
| EPS | Mapato kwa hisa |
| IASB | Bodi ya Viwango ya Uhasibu ya Kimataifa |
| IESBA | Bodi ya Viwango ya Maadili ya Kimataifa ya Wahasibu |
| IFRS | Viwango vya Kimataifa vya Taarifa za Fedha |
| LC | Barua za mikopo |
| LDR | Mkopo kwa uwiano wa Amana |
| LGD | Hasara itokanayo na mkopo usiolipika |
| NPL | Mikopo chechefu |
| POCI | Mali zinazotarajiwa kuingiza hasara |
| ROUA | Haki ya Matumizi ya Mali |
| SGL | Ukopaji wa Vikundi |
| SICR | Ongezeko Kubwa la Hatari ya Mikopo |
| SME | Wafanyabiashara wadogo na kati |
| SMR | Kiwango cha Chini cha Amana cha Kisheria |
| SPPI | Malipo ya Kianzio na Riba |
| SPV | Kampuni ya makusudio maalum |
| TMRC | Taasisi ya Mikopo ya Nyumba ya Tanzania |
| TZS | Shilingi ya Kitanzania |
| USD | Dola ya Marekani |



# Taarifa ya mkutano mkuu wa ishirini na mbili wa wanahisa

## KARIBU MKURUGENZI MTENDAJI - SABASABA MOSHINGI



Bodi ya Wakurugenzi ya DCB Commercial Bank PLC ina furaha kumtambulisha kwenu Bw. Sabasaba Kitewita Moshingi ambaye ni Afisa Mtendaji Mkuu na Mkurugenzi Mtendaji mpya wa Benki, kuanzia tarehe 1 Novemba 2023.

Bw. Sabasaba Kitewita Moshingi ana uzoefu wa zaidi ya miaka 20 katika sekta ya benki, akiwa ameshika nyadhifa za juu katika benki za ndani na za kimataifa, akiwa na utaalamu wa kipekee katika maeneo kama vile Uendeshaji wa Benki, Fedha, Biashara, Mikopo na Huduma kwa Wateja.

Kabla ya kujiunga na DCB Commercial Bank, Bw. Sabasaba aliwahi kuwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Tanzania Commercial Bank kwa zaidi ya miaka 12, ambapo uongozi wake ulitoa mchango mkubwa katika ukuaji na mafanikio ya taasisi hiyo.
DCB Commercial Bank inaendelea kujitolea kuwaarifu washirika na wadau wetu kuhusu maendeleo muhimu. Tuna imani kuwa chini ya uongozi wa Bw. Sabasaba Kitewita Moshingi, Benki itafikia viwango vipya vya mafanikio na ukuaji.

Tunashukuru kwa kuendelea kwenu kutuamini na kutuunga mkono

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA ISHIRINI NA MBILI WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwamba, Mkutano Mkuu wa Ishirini na Mbili wa mwaka wa DCB Commercial Bank Plc, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 14 Septemba 2024 kwa njia ya mtandao, kuanzia saa nne kamili (4:00) asubuhi.

### AGENDA

22.1 Kuthibitisha akidi na kufungua mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
22.2. Kuridhia agenda ya Mkutano Mkuu wa 22 wa mwaka
22.3. Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka
22.4. Kupokea na kuridhia utekelezaji wa yatokanayo na Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka
22.5. Kupokea na kuridhia taarifa za Bodi ya Wakurugenzi na hesabu zilizokaguliwa za Mwaka 2023
 22.5.1 Taarifa ya wakurugenzi ya mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
 22.5.2 Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
 22. 5.3 Taarifa ya mkaguzi huru ya hesabu zilizokaguliwa za mwaka ulioishia tarehe 31 Disemba, 2023
22.6. Kupokea na kuidhinisha pendekezo la kuongeza mtaji wa benki kwa njia ya hisa stahiki
22.7. Kupokea taarifa ya Kuisha kwa muda, Kuongeza muda na uteuzi wa wajumbe wa Bodi
22.8. Kuteua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 31 Disemba 2024
22.9. Kupokea na kuridhia pendekezo la malipo ya ada kwa wajumbe wa bodi
22.10. Kupanga tarehe ya Mkutano Mkuu wa 23 wa mwaka
22.11. Mengineyo
22.12. Kufunga mkutano

### MAELEKEZO

1. Wanahisa wanaotarajia kuhudhuria mkutano mkuu wanatakiwa wawe na CDS namba ambazo zinapatikana kwenye risiti ya uwekezaji wa hisa (depository receipt) au taarifa ya akaunti (CSDR account statement).

2. Wanahisa ambao hawataweza kuhudhuria Mkutano wanaruhusiwa kuchagua wawakilishi watakaohudhuria na kupiga kura kwa niaba yao kwa kufuata/kuzingatia sheria na Katiba ya Kampuni. Fomu ya uwakilishi (Proxy Form) lazima ijazwe na kuwasilishwa kwenye ofisi ya Katibu wa Benki iliyopo Makao Makuu ya Benki ya DCB au kwa njia ya mtandao kupitia barua pepe shareholder@dcb.co.tz au matawini kabla ya saa 4 asubuhi siku ya Ijumaa tarehe 13 Septemba 2024.

3. Nakala za taarifa ya mwaka na fomu za mwakilishi (proxy forms) zitapatikana matawini na kwenye tovuti ya benki (www.dcb.co.tz).

4. Kufungwa kwa orodha (Register) ya wanahisa tarehe 11 Septemba 2024

5. Mapendekezo ya wanahisa yawasilishwe kwenye ofisi za makao makuu zilizoko jengo la DCB Magomeni Mwembechai au kwa barua pepe kabla ya saa 8.00 mchana siku ya Alhamisi tarehe 12 Septemba 2024.

Kwa idhini ya bodi,



Regina Mduma
**Katibu wa kampuni**

# Kuthibitisha kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka



Muhtasari wa mkutano mkuu wa 21 wa wanahisa wa benki ya DCB uliofanyika tarehe 17 Juni 2023 katika ukumbi wa kimataifa wa Julius Nyerere

## WAJUMBE WA BODI WALIOHUDHURIA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bw. Alexander Sanga | Mwenyekiti wa Mkutano |
| 2. | Bw. David Shambwe | Mjumbe wa Bodi |
| 3. | Dkt. Amina Baamary | Mjumbe wa Bodi |
| 4. | Bw. Cliff Maregeli | Mjumbe wa Bodi |
| 5. | Bw. Isidori Msaki | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji |
| 6. | Bi. Regina Mduma | Katibu wa Kampuni |

## WAJUMBE WA BODI WALIOTOA UDHURU

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bi. Pamela Nchimbi | Mjumbe wa Bodi |
| 2. | Bi. Hanifa Hamza | Mjumbe wa Bodi |

## WAKURUGENZI WAANDAMIZI WA BENKI YA DCB

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Isidori Msaki | Kaimu Mkurugenzi Mtendaji |
| 2. | Deusdethit Mulindwa | Mkurugenzi wa Idara ya Fedha |
| 3. | Nelson Swai | Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji |
| 4. | Regina Mduma | Mkurugenzi wa Idara ya Sheria na Katibu wa Benki |
| 5. | Deogratius Thadei | Mkaguzi Mkuu wa Ndani |
| 6. | Msingo Mkanzabi | Mkurugenzi wa Idara ya rasilimali watu |
| 7. | Haika Machaku | Mkurugenzi wa Idara ya Mikopo Midogo Midogo |
| 8. | Maria Mduda | Kaimu Mkurugenzi wa Mikopo |
| 9. | Ruth Mpangalala | Kaimu Mkurugenzu wa Biashara |
| 10. | Rahma Ngassa | Mkurugenzi wa Idara ya Masoko na huduma kwa wateja |
| 11. | Emmanuel Mushi | Kaimu Mkurugenzi wa Udhibiti wa Viashiria Hatarishi |

## WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WAANZILISHI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Matao Adolfu | Halmashauri ya Jiji la Dar-es-Salaam |
| 2. | Matao Adolfu | Halmashauri ya Manispaa ya Ilala |
| 3. | Onesmo Mwonga | Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni |
| 4. | Japhet Lutambi | Halmashauri ya Manispaa ya Ubungo |
| 5. | Faraja Makua | Halmashauri ya Manispaa ya Temeke |
| 6. | Godfrey Martin | Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni |

## WAWAKILISHI KUTOKA KUNDI LA WANAHISA WA TAASISI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Fredrick Lushinge | UTT – Amis |
| 2. | Celestine Muganga | National Health Insurance Fund (NHIF) |

## WANAHISABINAFSI

**Orodha imeambatanishwa kama Kiambatanisho**

## WAALIKWA

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Alex G. Mgongolwa | Mwanasheria Mshauri wa DCB |
| 2. | Patrick Kiambi | Wakaguzi Huru – Pricewaters Cooper |
| 3. | Cletus Kiyuga | Wakaguzi Huru – Pricewaters Coopers |
| 4. | Athony Kashube | Mamlaka ya Masoko ya Mtaji na Dhamana (CMSA) |
| 5. | Happy Mushi | Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) |

## UTANGULIZI

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Bw. Isidori Msaki aliwakaribisha wanahisa na waalikwa wote waliofika kwenye Mkutano Mkuu wa Ishirini na Moja wa Mwaka na kuwashukuru kwa kuweza kufika kwenye Mkutano huo. Baada ya hapo alitoa utambulisho wa Bodi ya Wakurugenzi, menejimenti ya DCB na wageni waalikwa.

### KUTHIBITISHA AKIDI NA KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA

Katibu wa benki akishirikiana na mwanasheria wa benki walitoa taarifa kwamba, Mkutano Mkuu wa Mwaka ni takwa la kisheria ya makampuni Tanzania na Katiba ya benki ya DCB. Taarifa ya mkutano inatakiwa kuwafikia wanahisa angalau siku 21 kabla ya Mkutano huo.

Mwanasheria Mshauri wa benki alithibitisha kwamba Taarifa ya Mkutano ilitolewa magazetini, kwenye mitandao ya kijamii, tovuti ya benki na kwa ujumbe mfupi wa simu kwa wanahisa wote kwa wakati, angalau siku ishirini na moja kabla la Mkutano Mkuu wa 21. Mwanasheria Mshauri wa benki alieleza kwamba Mkutano Mkuu wa 21 wa mwaka unahitaji akidi ya asilimia 75 na tayari kulikuwa na wanahisa wenye umiliki wa hisa wa takribani asilimia 85, akidi ilithibitishwa kutimia.

### KURIDHIA AGENDA YA MKUTANO MKUU WA 21 WA MWAKA

Wajumbe waliridhia agenda za Mkutano Mkuu wa ishirini na moja wa mwaka kama zilivyoorodheshwa kwenye taarifa ya Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 21 wa benki na kitabu cha Mkutano Mkuu wa Mwaka wa 21.

### KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA 20 WA MWAKA

Mwanasheria Mshauri alieleza kwamba, kwa kuwa Katibu wa Kampuni hajapokea mapendekezo yeyote ya mabadiliko ya ajenda, basi ajenda iliyopo kwenye Taarifa ya Mkutano Mkuu wa 21 ndio ajenda ya kikao hicho. Wanahisa walihojiwa na kukubaliana na ajenda hiyo.

### KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANO MKUU WA 20 WA MWAKA

**ILIRIPOTIWA** kwamba agizo la wanahisa kwa Bodi ya Wakurugenzi katika kuongeza mapato yasiyotokana na riba, ili kupunguza athari zinazitokana na mikopo chechefu, benki imefanyia kazi agizo hilo na kwa mwaka wa mahesabu 2022 mapato hayo yaliongezeka kwa kiasi cha asiliia 49 ya mapato yote ya benki.

**ILIRIPOTIWA** kwamba agizo la wanahisa kwa Bodi ya Wakurugenzi kuhakikisha kwamba benki ina akaunti maalum za wanahisa zinatakazotumika kufanya shughuli za kibenki ikiwa ni pamoja na kuingiziwa gawio ili kuisaidia benki kukua, benki imeweza kufungua account hizo ambapo kila mwanahisa analipiwa magawio yake kupitia akaunti hizo.

**ILIRIPOTIWA** kwamba agizo la wanahisa kwa Bodi ya Wakurugenzi kuhakikisha ripoti ya mahesabu inawashilishwa kwa lugha ya Kiswahili lilitekelezwa na ripoti ya mahesabu ya mwaka 2022 imewakilishwa kwa lugha ya Kiswahili.

### KUPOKEA NA KURIDHIA TAARIFA ZA BODI YA WAKURUGENZI NA HESABU ZILIZOKAGULIWA ZA MWAKA 2022

Wanahisa walipokea taarifa kutoka kwa Bodi ya Wakurugenzi ambayo imegawanyika kwenye makundi manne; barua ya mwenyekiti wa bodi, barua ya mkurugenzi mtendaji, taarifa za fedha za mwaka ulioishia 31 Disemba 2022 na taarifa ya Mkaguzi Huru wa mahesabu kwa mwaka ulioishia 31 Disemba 2022.

**ILIRIPOTIWA** kwamba jumla ya wakurugenzi nane (8) akiwamo Mkurugenzi Mtendaji walihudumia benki katika kipindi hicho na hakuna Mkurugenzi aliyemiliki zaidi ya asilimia 5 ya jumla ya mtaji wa hisa wa Benki. Bodi ya Wakurugenzi iliendelea kuwajibika katika kuhakikisha kwamba taratibu na kanuni zake zote zinazingatiwa kwa mujibu wa taratibu za uendeshaji wa Benki.

Wanahisa walipokea taarifa ya mabadiliko ya uongozi katika bodi ya wakurugenzi kwamba Bw, Maharage Chande aliyekuwa mjumbe na mwenyekiti wa Bodi amestaafu katika nyadhifa hizo ndani ya benki ya DCB. Na kadhalika, Bw. Godfrey Ndalahwa aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Benki amemaliza muda wake na nafasi hiyo imeshikiliwa kwa muda na Bw. Isidori Msaki wakati aliyetuliwa na Bodi ya Wakurugenzi Bw. Sabasaba Moshingi anajiandaa kuripoti.

Wanahisa waliarifiwa kwamba mkaguzi huru wa benki (PriceWatersCoopers) alifanya mabadiliko ya mahesabu ya mwaka 2021 na kukagua mahesabu ya mwaka 2022. Hivyo taarifa ya hesabu ilionyesha waraka wa mizania kwa kuonyesha hesabu zilizokaguliwa za mwaka 2022, hesabu zilizorejewa za mwaka 2021 na hesabu zilizorejewa za mwaka 2020.

**ILIRIPOTIWA** Kwamba kwa mwaka 2022 Benki ilipata faida kabla ya kodi ya Tsh 967.3 milioni ikilinganishwa na hasara ya Tsh 2.1 bilioni kwa mwaka 2022. Vipimo vingine vya utendaji vya benki vilikuwa kama ifuatavyo: -

Benki ilipata jumla ya mapato ya mwaka kabla ya tengo la mikopo chechefu la Tsh 15.2 bilioni, ikiwa imepungua kidogo ikilinganishwa na Tsh 16.1 bilioni zilizoripotiwa mwaka 2021.

Jumla ya mali za benki ziliongezeka kutoka Tsh 172.8 bilion (2020), Tsh 192.4 bilioni (2021) hadi kufikia Tsh 211.9 bilioni (2022).

Mikopo halisi ilikuwa Tsh 98.07 bilioni (2020), Tsh 114.71 Bilioni (2021) na kiasi cha Tsh 120.84 Bilioni (2022). Hata hivyo, uwiano wa mikopo Chechefu uliripotiwa kuwa wa asilimia 12.2% kwa mwaka 2022, ikilinganishwa na asilimia 11.1% iliyoripotiwa mwaka 2021.

Jumla ya gharama za uendeshaji zilikuwa kiasi cha Tsh 20.6 bilioni (2022) kutoka Tsh 18.7 bilioni (2021). Amana za wateja zilifikia Tsh141.9 bilioni, ikiwa ni ongezeko kutoka Tsh 125.2 bilioni zilizoripotiwa mwaka uliotangulia. Jumla ya thamani ya hisa iliongezeka hadi kufikia TZS 28.4 bilioni kutoka TZS 27.5 bilioni zilizoripotiwa mwaka uliotangulia.

**ILIRIPOTIWA** kwamba Bodi ya Wakurugenzi ilifanya tathimini kuhusu uwezo wa Benki kuendelea kufanya biashara na matokeo yaliyoripotiwa kwamba Bodi imejiridhisha Benki itaweza kufanya shughuli zake kwa muda mrefu kwani ina mtaji wa kutosha na mikakati dhabiti ya kuongeza kipato cha benki.

**ILIRIPOTIWA** kwamba Bodi ya Wakurugenzi haikupendekeza malipo ya gawio kwa wanahisa kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2022 kwasababu benki haikukidhi vigezo vya Uwiano wa Gharama za Uendeshaji na Mapato Ghafi wa asilimia 55 na mikopo chechefu ya asilimia 5, vilivyoainishwa na Benki Kuu ya Tanzania ili kupata malipo ya gawio.

**ILIRIPOTIWA** kwamba benki ya DCB ilishirikisha wadau wakuu ikiwemo kampuni za mitandao ya simu, kampuni za mifumo ya kitechnologia za kifedha na ilizindua bidhaa na huduma mpya katika robo ya pili na ya tatu ya mwaka 2022 kama ushahidi wa ushirikiano wake na wadau hao ikiwa ni pamoja na Tigo Lipa kwa simu na Selcom Pay (MasterPass QR).

Taarifa ilitolewa kwamba mapato halisi ya riba kwa mwaka 2022 yalikua Tsh bilioni 15.2 ambapo kiasi cha Tsh bilioni 3.8 kilitolewa kama ongezeko la tengo katika mikopo. Jumla ya mapato yasiyo ya riba yaliongezeka kutoka kiasi cha Tsh bilioni 6.8 mwaka 2021 kufikia Tsh bilioni 10.2 mwaka 2022.

Wanahisa walitaarifiwa kwamba mali za benki ziliongezeka mwaka hadi mwaka, yaani, Tsh bilioni 172.8 (2020), Tsh bilioni 192.4 (2021) na Tsh bilioni 211.9 (2022). Kadhalika dhima za benki kabla ya kuongeza dhamani ya hisa ziliendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka; Tsh bilioni 143.4 (2020), Tsh bilioni 164.8 (2021) na Tsh bilioni 183.4 (2022) lakini kutokana na mikopo chechefu, faida ya mwaka ilipungua kwa kiasi cha shilingi bilioni 3.8.

Taarifa ilitolewa kwamba kwa mujibu wa sheria za benki kuu, kila benki inatakiwa kufikia uwiano wa gharama na matumizi usiopungua asilimia 55%. Benki imejiwekea mpango mkakati wa kufikia uwiano huo ifikapo mwaka 2025, hivi sasa uwiano wa gharama na matumizi ni asilimia 79%. Pia benki inatakiwa kuwa kiwango cha 5% katika mikopo chechefu. Kupitia mpango mkakati mpya, benki ilitarajia kufikia kiwango hicho mwisho wa mwaka 2022.

Sehemu ya mwisho ya taarifa ya bodi ya wakurugenzi ilikuwa kupokea taarifa ya mkaguzi huru wa hesabu za mwaka 2022. Taarifa iliwakilishwa na muwakilishi kutoka PriceWatersCoopers (PWC) aliyeelezea kwamba taarifa zao zimezingatia kanuni za kimataifa za uhasibu, kanuni za benki kuu katika kuwakilisha mahesabu na sheria mbalimbali. Wakaguzi huru waliona kwamba benki inatakiwa kupunguza idadi ya mikopo chechefu na hilo liliweza kufanyika. Zaidi ya hapo walidhibitisha kwamba benki iko imara na walitoa hati safi.

Wanahisa walipokea taarifa za bodi ya wakurugenzi, walijadili na kutoa mapendekezo kama ifuatavyo:

**USHAURI** ulitolewa kwamba ripoti ya mahesabu inayohusiana na masuala ya utawala bora ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza ufanisi zaidi.

**SWALI** liliulizwa kwamba ni lini benki itafikia uwiano wa mikopo chechefu na mapato na matumizi kama ilivyo sheria ya Benki Kuu ili kuweza kulipa gawio kwa wanahisa.

**MAJIBU** yalitolewa kwamba benki ina mikakati itakayoiwezesha kufikia kiwango cha mikopo chechefu kinachokubalika na Benki Kuu kufikia mwisho wa mwaka 2023. Pia benki ina mikakati ya kupunguza gharama za uendeshaji ili iwezi kufikia uwiano wa gharama na matumizi unaokubalika na Benki Kuu.

**PENDEKEZO** lilitolewa kwamba ili kuongeza ufanisi katika bodi ya wakurugenzi, Bodi ijitahidi kutafuta mjumbe wa bodi katika tasnia ya Sheria.

## KUPOKEA NA KURIDHIA MABADILIKO YA VIFUNGU VYA KATIBA YA KAMPUNI

Wanahisa walipokea na kuridhia mabadiliko ya yafuatayo katika Katiba ya benki:Huduma za kibenki zinazotolewa kwa njia ya kielektroniki kama huduma za TISS, huduma za benki kwa njia ya simu, ATM na Internet Banking.Usajili wa alama za biashara na huduma, hataza na haki miliki zinazihusiana na bidhaa, huduma, nyenzo za kazi nakadhalika. Utaratibu wa kutumia hisa kama dhamana ya mkopo na taratibu za kuhamisha hisa. Njia mbalimbali zinazoweza kufanya Mkutano Mkuu wa Mwaka ikiwa ni pamoja na kufanya Mkutano Mkuu kwa njia ya Mtandao. Jinsi ya kuwakilisha agenda ya mengineyo ya Mkutano Mkuu wa Mwaka.Mwanahisa anayekidhi haki ya kupiga kura. Ongezeko la wajumbe huru wa Bodi kutoka 1 kufikia 2

## KUPOKEA TAARIFA YA KUISHA MUDA, KUONGEZA MUDA NA UTEUZI WA WAJUMBE WA BODI

Wanahisa waliazimia kuongeza muda wa kipindi kingine cha miaka mitatu kwa Bi. Zawadia Nanyaro kuanzia tarehe 1 Juni 2023 hadi tarehe 31 Mei 2026.

Wanahisa walimteua Prof. Thadeo Satta kuwa mjumbe wa Bodi wa benki kama Mkurugenzi Huru wa Bodi kwa kipindi cha miaka mitatu.

Wanahisa walijadili suala ya kuteua mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi. Bodi ya wakurugenzi iliomba kukaimishwa mamlaka ya uteuzi wakati benki inasubiri majibu kutoka Benki Kuu kuhusiana na suala la kumthibitisha (vetting) Mkurugenzi aliyefanyiwa usaili na Bodi ya Wakurugenzi katika hiyo nafasi. **AZIMIO** lilitolewa kwamba kwa kuwa mkurugenzi huyo anawakilisha kundi la wanahisa binafsi, uteuzi wake ufanywe na wanahisa wenyewe kupitia Mkutano Mkuu.

## KUTEUA MKAGUZI HURU WA MAHESABU KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2023

Wajumbe walijulishwa mchakato uliofanya wa kumchagua mkaguzi huru wa hesabu kwa mwaka 2023 na utayari wa PriceWaterhouseCoopers (PWC) kuendelea na ukaguzi wa mahesabu ya mwaka 2023. Bodi ilipendekeza PriceWatersCoopers (PWC) kuteuliwa kama mkaguzi huru kwa mwaka 2023 kwa gharama za Tsh, 150,000,000.Wajumbe waliridhia pendekezo hilo na kumteua PriceWaterhouseCoopers (PWC) kama mkaguzi huru wa mahesabu kwa mwaka wa fedha ulioishia 31 Disemba 2023.

## KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA MALIPO YA ADA KWA WAJUMBE WA BODI

Wanahisa waliazimia kuridhia mapendekezo ya Bodi kuwa malipo ya ada kwa Wajumbe wa Bodi yaendelee kuwa Tsh 6,000,000 baada ya kodi kwa mwaka kwa kila Mjumbe wa Bodi.

## KUPOKEA TAARIFA YA GAWIO LA MWAKA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA 2022

**IMERIPOTIWA** kwamba kutokana na sheria mpya ya Benki Kuu ya Tanzania, benki inatakiwa kuwa na mikopo chechefu isiyozidi asilimia 5 na mizania ya mapato na matumizi isiyozidi asilimia 55. Hadi kufikia mwisho wa mwaka 2022 benki ilikuwa na asilimia 12.2 ya mikopo chechefu hivyo haijafikia matakwa ya kisheria na hivyo kupelekea Bodi ya wakurugenzi kupendekeza kwa wanahisa kutokutoa gawio kwenye faida iliyopatikana mwaka wa fedha 2022.

Baada ya kujadili swala zima la gawio wanahisa waliridhia pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi la kutokulipa gawio kwa mwaka wa mahesabu unaishia tarehe 31 Disemba 2022 na kutumia faida baada ya kodi ya Tsh 747 milioni kuongeza mtaji wa benki.

## MENGINEYO

**IMERIPOTIWA** kwamba hakukuwa na agenda ya mengineyo iliyowakilishwa kwa Katibu wa Kampuni kabla ya Mkutano Mkuu na pia wanahisa hawakuwa na mengineyo yeyote.

Mkutano ulifungwa saa 8:00 mchana.

Zawadia Nanyaro  Tarehe; 14 09 2024
**Mwenyekiti**

Regina Mduma  Tarehe: 14 09 2024
**Katibu wa Kampuni**

## 22.4 KUPOKEA NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA YATOKANAYO NA MKUTANAO MKUU WA 21 WA MWAKA

Yatokanayo na mkutano mkuu wa 21 uliofanyika tarehe 17 Juni 2023

| NA | AGIZO | UTEKELEZAJI |
|---|---|---|
| 1 | Ripoti ya mahesabu inayohusiana na masuala ya utawala bora ifanyiwe marekebisho kwa kuongeza ufanisi zaidi | Hii imetekelezwa na marekebisho kujumuishwa kwenye ripoti ya mahesabu ya mwaka 2023. |
| 2 | Uteuzi wa Mkurugenzi anayewakilisha kundi la wanahisa binafsi ufanywe na wanahisa wenyewe kupitia Mkutano Mkuu. | Agizo limetekelezwa Mkurugenzi atakaewakilisha kundi la wanahisa binafsi ameletwa kwenye mkutano huu kwaajili ya uteuzi. |

## 22.5 KUPOKEA TAARIFA WAKURUGENZI WA BODI



### UJUMBE KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BODI

**Wapendwa Wanahisa,**

Kwa heshima na taadhima na kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi, napenda kuwakaribisha katika Mkutano Mkuu wa 22 wa Mwaka. Ninayo furaha kuwasilisha kwenu ripoti ya utendaji wa benki ya mwaka wa fedha 2023. Ripoti hii imejumuisha mafanikio yetu, changamoto, na mpango mkakati wetu unaoendeleza dhamira na maono ya DCB.

Katika mwaka 2023, DCB ilistahimili mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi na kiutendaji. Licha ya hayo benki ilikuza mizania yake kwa asilimia 9, ilipunguza mikopo chechefu kwa asilimia 50 kutoka uwiano wa asilimia 12 hadi 6, na mwenendo wa amana ulisalia kuwa chanya mwaka mzima. Matokeo ya kina ya utendaji ya mwaka wa 2023 yanapatikana kwenye ukurasa 28 hadi 32 wa Ripoti ya Mwaka.

Ndugu wanahisa, katika mwaka wa 2023, tulitekeleza mipango ya kimkakati ambayo imeimarisha nafasi yetu sokoni na kuboresha huduma zetu. Mafanikio na maendeleo muhimu ya benki yetu mwaka 2023 ni pamoja na:

**DCB-TigoWakala:** Ili kuongeza upatikanaji wa huduma za benki kwa wateja wetu, benki iliingia makubaliano na Tigopesa ili kuruhusu wateja wa DCB kutumia wakala Tigopesa kupata huduma za kuweka na kutoa pesa. Kupitia ubunifu huu wateja wa DCB, sasa wanafurahia upatikanaji wa huduma za benki kwa urahisi zaidi katika maeneo mengi nchini.

**DCB Vicoba App:** Benki ilizindua mfumo wa kidijitali wa uendeshaji wa Vicoba ili kuweka bayana na kuboresha utunzaji wa taarifa za vikundi. Mfumo huu unaunganisha wanachama wa vikundi na benki na kuwawezesha kukopa, kutunza amana na kufanya miamala, kusajili wanachama wapya, kufatilia marejesho na michango. Mfumo huu unapunguza gharama za uendeshaji wa Vicoba na upatikaji wa huduma za benki kwa vikundi kwa vigezo nafuu.

**Mabadiliko ya Uongozi:** Bodi ilifanya mabadiliko katika nafasi muhimu za uongozi ili kufanikisha malengo ya benki. Bodi ilimteua Mkurugenzi Mtendaji, Bwana Sabasaba Moshingi. Bwana Moshingi alijiunga rasmi na benki ya DCB Novemba 2023, akiwa na uzoefu wa zaidi ya miaka 30 katika tasnia ya benki. Bwana Moshingi ameonyesha mafanikio makubwa katika kubadilisha benki ndogo kuwa benki za daraja la kwanza, na Bodi inaamini uzoefu wake utatumika katika kuleta mafanikio chanya katika benki yetu na kusimama utekelezaji wa mpango mkakati wa miaka mitano 2024 -2028. Kwa uongozi wa sasa, Bodi ina uhakika kwamba maono ya kimkakati ya benki yatatekelezwa ili kuongeza thamani kwa wanahisa wake.

Licha ya mafanikio hayo, ni muhimu kutambua kwamba benki ilikumbana na changamoto mbalimbali katika mwaka 2023, ikiwa ni pamoja na upungufu wa fedha za kigeni, mfumuko wa bei ya mafuta, kuongezeka kwa gharama za riba, kushuka kwa viwango vya riba za mikopo, tengo la mikopo chechefu na mabadiliko ya uongozi wa benki yaliyoanza mwishoni mwa 2022.

Bodi na Uongozi wameandaa mpango mkakati mpya wa miaka mitano kutoka 2024 hadi 2028 kuhakikisha ukuaji endelevu wa benki. Maeneo muhimu ya mkakati huo ni pamoja na kukuza mtaji wa benki kufikia TZS bilioni 61, ukuaji wa amana, ukuaji na ubora mikopo, utoaji wa huduma za kibenki kwa wenye kipato cha chini, na uboreshaji wa njia za utoaji huduma.

Mkakati huu mpya wa utawezesha ukuaji wa mizania kufikia nusu trilioni, ongezeko la faida kufikia jumla ya TZS bilioni 37 bilioni kufikia mwaka 2028, kufikia uwiano wa ufanisi wa gharama wa asilimia 54 pamoja na kudumisha kiwango cha mikopo chechefu chini ya asilimia 4.5.

Tunapotafakari mafanikio na changamoto za mwaka 2023, ninatoa shukurani zangu za dhati kwa wanahisa wetu, wasimamizi, na taasisi za serikali kwa kuendelea kuwa na imani na benki yenu na kutuunga mkono katika biashara.

Kwa wateja wetu, tunashukuru kwa kutuamini, kutumia huduma zetu na kutupa maoni ili kuendelea kuifanya DCB kuwa mkombozi wa kweli.

Pia napenda kuwapongeza wajumbe wenzangu wa bodi ya Wakurugenzi, kwa ushirikiano wenu usio na kifani, mwongozo na maarifa ya kimkakati katika kuhakikisha kuwa mkakati wa benki unatekelezwa.

Mwisho, nawashukuru sana wafanyakazi wetu, ambao kazi yao imekuwa na mchango mkubwa katika safari ya mabadiliko ya benki yetu.Nina uhakika mkakati wetu thabiti wa miaka mitano utaiweka DCB katika nafasi nzuri ya kukabiliana na changamoto na na kuzifanya kuwa fursa ambazo zitaiwezesha benki kuwa kinara na kuongeza thamani kwa wanahisa wake. Kwa pamoja, tuendelee kushirikiana kutekeleza dhamira yetu ili kufanikisha malengo ya benki.Asanteni kwa kutuunga mkono na kuendelea kuwa na imani na benki yetu.



Zawadia Nanyaro
**Mwenyekiti Wa Bodi**



## UJUMBE KUTOKA KWA MKURUGENZI MTENDAJI

Wapendwa Wanahisa, kwanza kabisa, napenda kutoa shukrani zangu za dhati hasa kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa kunipa fursa ya kuhudumu katika benki yetu kama Mkurugenzi Mtendaji. Mimi na watendaji wenzangu tumedhamiria kuandika upya historia ya Benki ya Biashara ya DCB na kuirejesha benki hii katika zama zake za utendaji bora na mafanikio ya kibiashara.

Napenda kuwasilisha kwenu Taarifa ya Fedha ya mwaka 2023. Licha ya ongezeko la mizania kutoka TZS bilioni 211 mwaka 2022 hadi TZS bilioni 231 mwaka 2023, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 9 kwa mwaka, benki ilirekodi hasara baada ya kodi ya TZS bilioni 3.6. Hasara hii ilitokana na ongezeko kubwa la gharama za riba kufuatia changamoto za ukwasi zilizoikumba sekta ya kibenki pamoja na ongezeko la tengo la mikopo chechefu.

Bodi ya wakurugenzi na menejimenti ya benki ilifanya uamuzi wa makusudi wa kuisafisha mizania tunapoanza safari ya mageuzi ya kubadii historia ya benki, jambo ambalo liliathiri kwa kiasi kikubwa utendaji wetu wa kifedha kwa mwaka 2023. Hivyo ikaja na mpango mkakati wa miaka mitano 2024-2028 unaolenga kukabiliana na changamoto hizi.

### Matokeo ya utendaji wa Benki

Benki ilifanikiwa kukuza mizania kwa 9% mwaka kwa mwaka kutoka TZS bilioni 211.9 hadi TZS bilioni 230.9. Uwekezaji katika masoko ya fedha (Hati fungani) uliongezeka kwa asimilia 38. Amana kutoka benki na taasisi za kifedha ziliongezeka kwa asilimia 99. Uwiano wa mikopo chechefu ulipungua kutoka asilimia 12 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 6 mwaka 2023. Licha ya mafanikio hayo benki ilipata hasara baada ya kodi ya TZS bilioni 3.6 kwa mwaka 2023.

### Mtazamo mpya na ukuaji endelevu wa Benki

Wapendwa wanahisa, kwa matumaini makubwa napenda kuwaletea maono yetu ya kimkakati ya miaka mitano ijayo (2024-2028). Mpango mkakati huu umejikita katika dhamira yetu ya kuhakikisha kwamba huduma za benki zinaboreshwa, ukuaji endelevu, ujumuishaji wa kifedha na kuongeza thamani ya biashara yetu kwa wadau wetu.

Vipaumbele vyetu vya kimkakati kwa miaka ijayo vimejikita katika mambo makuu matano: Ukuaji wa mtaji, Ukuaji wa amana za wateja, Ubora wa mikopo na ukuaji wa mapato, kutanua wigo na ufanisi wa utoaji huduma, na Mikopo kwa wateja wa kipato cha chini.

### Ukuaji wa Mtaji

Kusudio la kuimarisha mtaji linatokana na takwa la kisheria inayoilazimu benki kuongeza mtaji wa angalau Tzs 10 Bilioni kabla ya mwisho wa mwaka 2024 kupitia hisa stahiki. Ongezeko hili litapelekea kujenga msingi imara wa mtaji unaokidhi malengo yetu ya ukuaji na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma zetu.

Kupitia ongezeko hili, benki itaongeza uwezo wake wa kutoa mikopo, kuwekeza katika teknolojia za kisasa, na kuboresha utoaji wa huduma.

### Ukuaji wa Amana za Wateja

Mkakati wetu wa ukuaji wa amana utazingatia kuongeza amana nafuu kutoka uwiano wa sasa wa 30:70 hadi kufikia zaidi ya 40:60 ifikapo mwaka 2028. Hii itafikiwa kupitia kudumisha mahusiano yetu na wanahisa waanzilishi, yaani manispaa ya mkoa wa Dar es salaam, wanahisa wa taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za serikali, wanahisa wengine na wafanyabiashara mbalimbali.Pia takribani vikundi 4000 vipya vya VIKOBA vinatarajiwa kujiunga na benki yetu.

Tutashirikiana na mifuko ya hifadhi ya jamii katika kuzindua bidhaa za zitakazo wasaidia wastaafu kupata huduma za kibenki na kuendeleza miradi yao.

### Uboreshaji wa mifumo ya kutolea huduma.

Mkakati wetu unatilia mkazo kuendelea kuimarisha mifumo yetu ya kutolea huduma kwa wateja. Tunapanga kufungua matawi sita mapya na kuhamisha matawi matatu na kuyapeleka kwenye maeneo yenye fursa zaidi za biashara. Uboreshaji huu utaimarisha upatikanaji wa huduma za zetu kwa wateja wengi zaidi.

Safari yetu ya mabadiliko ya kidijitali itaendelea na uboreshaji wa huduma zetu kupitia simu za mkononi, mawakala wa benki, Intanet na ATM. Uboreshaji huu utaongeza ufanisi, unafuu na ubora wa huduma kwa wateja.

### Ubora na ukuaji wa mikopo na Mapato

Mkakati wetu wa ukuaji wa mikopo unalenga kukuza mikopo hadi TZS bilioni 322 ifikapo mwaka 2028 huku tukidhibiti uwiano wa mikopo chechefu chini ya asilimia 4.5. Ukuaji huu utachagizwa na ukuaji katika mikopo ya biashara, mikopo binafsi,na mikopo ya wafanyakazi. Tunatarajia kuongeza utoaji wa mikopo kwa wajasiliamali wadogo wadogo ikiwemo makundi maalumu hadi kufikia kiasi cha TZS bilioni 50 wakati mikopo ya kibiashara inatarajiwa kufikia hadikiasi cha TZS bilioni 186 mpaka kufikia mwaka 2028.

### Mikopo kwa wajasiriamali wadogo wadogo na wa kati

Katika msingi wa dhamira yetu ni kutoa huduma za fedha jumuishi. Tutaongeza huduma zetu za mikopo ya microcredit ili kuwahudumia vizuri watu wenye mapato ya chini, hasa wanawake na vikundi vya vijana. Kwa kuendeleza bidhaa za akiba na mikopo zilizobinafsishwa, tunalenga kukidhi mahitaji maalum ya makundi haya ambayo hayajahudumiwa vya kutosha.

### Hitimisho

Ningependa kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanahisa wetu, wateja, wafanyakazi, na wadau wengine wote kwa kutuamini, kutupa ushirikiano na kujitolea ili kuiendeleza benki yetu.

Pamoja tushikamane kuimarisha benki yetu ili iwe bunifu katika utoaji huduma zenye ubora, uendelevu ili kuwawezesha wateja wetu na jamii kwa ujumla kustawi.

Kwa heshima,



Sabasaba Moshingi
**Mkurugenzi Mtendaji**

# TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA ULIOISHA 2023

| | Notes | 2023 TZS'000 | 2022 TZS'000 |
|---|---|---|---|
| Mapato ya Riba | 8 | 27,835,426 | 28,607,305 |
| Gharama za Riba | 9 | (15,085,920) | (13,380,278) |
| **Mapato halisi ya Riba** | | **12,749,506** | **15,227,027** |
| Ongezeko la tengo katika mikopo | | (3,109,550) | (3,874,865) |
| **MAPATO HALISI YA RIBA BAADA YA ONGEZEKO LA TENGO KATIKA MIKOPO** | | **9,639,956** | **11,352,162** |
| Mapato ya ada na kamisheni | 10 | 4,880,621 | 5,751,715 |
| Mapato ya fedha za kigeni | 11 | 364,191 | 386,107 |
| Mapato mengine | 12 | 1,232,897 | 4,144,391 |
| **Jumla ya mapato yasiyo ya Riba** | | **6,477,709** | **10,282,213** |
| **JUMLA YA MAPATO YA KIUENDESHAJI** | | **16,117,665** | **21,634,375** |
| **GHARAMA ZA UENDESHAJI** | | | |
| Gharama za wafanyakazi | 13 | (10,042,148) | (9,993,648) |
| Gharama za ujumla za kiutawala | 14 | (6,817,215) | (8,052,221) |
| Kupungua kwa thamani na kupungua kwa madeni | 15 | (3,852,255) | (2,621,158) |
| **JUMLA YA GHARAMA ZA UENDESHAJI** | | **(20,711,618)** | **(20,667,027)** |
| **FAIDA/(HASARA) KABLA YA MAKATO YA KODI** | | **(4,593,953)** | **967,348** |
| Kodi ya mapato | 19 | 975,721 | (219,645) |
| **FAIDA/(HASARA ) BAADA YA KODI YA MAPATO** | | **(3,618,232)** | **747,703** |
| Thamani ya faida/(hasara) katika uwekezaji | | | |
| **Jumla/(hasara) ya mapato yote kwa mwaka** | | **(142,542)** | **142,542** |
| Jumla/hasara) ya mapato kwa mwaka | | **(3,760,774)** | **890,245** |
| Mapato/(hasara) kwa hisa | 34 | **(37.05)** | **7.66** |

# TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI DISEMBA 31 2023

| | Noti | 2023<br>TZS'000 | 2022<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Mali** | | | |
| Fedha taslim na salio na Benki Kuu ya Tanzania | 20 | 21,576,928 | 19,005,746 |
| Uwekezaji katika amana za serikali | 22 | - | 27,639,102 |
| Uwekezaji katika amana za serikali | 22 | 57,156,768 | 13,663,360 |
| Uwekezaji katika amana za hisa | 24 | 2,040,200 | 2,040,200 |
| Mikopo na vianzio kwa benki | 21 | 5,271,278 | 3,963,844 |
| Mikopo na vianzio kwa wateja | 23 | 120,403,894 | 120,847,669 |
| Kodi ya kampuni inayokusanyika | 28 | 975,000 | 2,095,060 |
| Mali ya kodi ya mapato iliyoahirishwa | 30 | 7,053,824 | 5,210,033 |
| Mali zingine | 27 | 3,001,042 | 3,230,825 |
| Haki ya matumizi ya mali zilizokodiwa | (i)36 | 6,890,965 | 5,494,196 |
| Mali na vifaa | 25 | 2,981,231 | 3,646,824 |
| Mali zisizoshikika | 26 | 3,631,022 | 5,067,216 |
| **Jumla ya mali** | | **230,982,152** | **211,904,075** |
| | | | |
| **Dhima** | dd | | |
| Amana kwa benki zingine | a.29 | 47,664,218 | 23,934,235 |
| Amana kutoka kwa wateja | b.29 | 140,053,421 | 141,941,494 |
| Mikopo | 31 | 11,213,836 | 11,900,791 |
| Dhima zingine | 32 | 2,862,953 | 2,774,670 |
| Dhima za ukodishaji | (ii)36 | 4,479,246 | 2,883,633 |
| **Jumla ya dhima** | | **206,273,674** | **183,434,823** |
| | | | |
| **Thamani ya hisa** | | | |
| Mtaji wa hisa | 33 | 24,061,904 | 24,061,904 |
| Mchango wa hisa | | 4,183,291 | 4,183,291 |
| Limbikiza la hasara | | (4,145,700) | (3,792,602) |
| HIfadhi ya hatari za jumla za benki | | 130,043 | 3,395,177 |
| Hifadhe ya uthamini wa mali | | 478,940 | 621,482 |
| **Jumla ya thamani ya hisa** | | **24,708,478** | **28,469,252** |
| | | | |
| **Jumla ya dhima na thamani ya hisa** | | **230,982,152** | **211,904,075** |

Taarifa za kifedha kwenye ukurasa wa 67 hadi 146 zilithibitishwa na kuidhinishwa kutolewa na Bodi ya Wakurugenzi 29 April 2024 na kusainiwa kwa niaba yake na:

Ms. Zawadia J. Nanyaro
**Chairperson**

Prof. Tadeo Satta
**Board Member**

# TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2023

| Year ended 31 December 2023 | Noti | MTAJI WA HISA | MCHANGO WA HISA | KIANZIO KUFIKIA MTAJI WA HISA | HIFADHI YA HATARI ZA JUMLA ZA BENKI | HIFADHI YA UTHAMINI WA HAKI | JUMLA YA MTAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **Katika tarehe 1 Januari 2023** | | **24,061,904** | **4,183,291** | **(3,792,602)** | **3,395,177** | **621,482** | **28,469,252** |
| Hasara ya mwaka | | - | - | (3,618,232) | - | - | (3,618,232) |
| Faida ya thamani halisi kwenye kifaa cha deni cha FVOCI | | - | - | - | - | (203,631) | (203,631) |
| Kodi ya mapato kwa faida ya thamani halisi | | - | - | - | - | 61,089 | 61,089 |
| **Jumla ya mapato ya jumla** | | **-** | **-** | **(3,618,232)** | **-** | **(142,542)** | **(3,760,774)** |
| Uhamishaji kwa/(kutoka) akiba ya hatari ya kanuni | | - | - | 3,265,134 | (3,265,134) | - | - |
| Gawio lililolipwa | | - | - | - | - | - | - |
| **Katika tarehe 31 Desemba 2023** | | **24,061,904** | **4,183,291** | **(4,145,700)** | **130,043** | **478,940** | **24,708,478** |

Akiba ya Hatari ya Benki kwa Mujibu wa Kanuni inawakilisha kiasi kilichowekwa kando ili kufidia ongezeko la akiba kwa hasara za mikopo zinazohitajika kutekeleza mahitaji ya miongozo ya uangalizi wa Benki ya Tanzania. Akiba hii haitumiwi kwa usambazaji..

# TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DISEMBA 2023

| Year ended 31 December 2022 | MTAJI WA HISA | MCHANGO WA HISA | KIANZIO KUFIKIA MTAJI WA HISA | HIFADHI YA HATARI ZA JUMLA ZA BENKI | HIFADHI YA UTHAMINI WA HAKI | JUMLA YA MTAJI | Total equity |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 | TZS'000 |
| **Katika tarehe 1 Januari 2022** | | **24,061,904** | **4,183,291** | **(4,751,930)** | **3,606,802** | **478,940** | **27,579,007** |
| Hasara ya mwaka | | - | - | 747,703 | - | - | 747,703 |
| Faida ya thamani halisi kwenye kifaa cha deni cha FVOCI | | - | - | - | - | 203,631 | 203,631 |
| Kodi ya mapato kwa faida ya thamani halisi | | - | - | - | - | (61,089) | (61,089) |
| **Jumla ya mapato ya jumla** | | **-** | **-** | **747,703** | **-** | **142,542** | **890,245** |
| Uhamishaji kwa/(kutoka) akiba ya hatari ya kanuni | | - | - | 211,625 | (211,625) | - | - |
| Gawio lililolipwa | | - | - | - | - | - | - |
| **Katika tarehe 31 Desemba 2022** | | **24,061,904** | **4,183,291** | **(3,792,602)** | **3,395,177** | **621,482** | **28,469,252** |


Akiba ya Hatari ya Benki kwa Mujibu wa Kanuni inawakilisha kiasi kilichowekwa kando ili kufidia ongezeko la akiba kwa hasara za mikopo zinazohitajika kutekeleza mahitaji ya miongozo ya uangalizi wa Benki ya**
..Tanzania. Akiba hii haitumiwi kwa usambazaji

# TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA KWA MWAKA ULIOISHA 2023

| | Noti | 2023<br>TZS'000 | 2022<br>TZS'000 |
|---|---|---|---|
| **Mtiririko wa fedha kutoka katika shughuli za uendeshaji** | | | |
| Faida kabla ya mapato ya kodi | | (4,593,953) | 967,348 |
| **:Imerekebishwa kwa ajili ya** | | | |
| Kushuka kwa thamani na kupungua kwa madeni | 15 | 3,852,255 | 2,621,158 |
| Gharama za riba katika mikopo | 31 | 984,669 | 929,893 |
| Mapato ya gawio | | (36,531) | (27,313) |
| Gharama za kifedha katika dhima za ukodishaji | | 30,554 | - |
| Mabadiliko mengine | | 4,965 | - |
| (Faida)/Hasara katika fedha za kigeni | (ii)36 | 326,917 | 242,244 |
| Mali zilizofutwa | | - | 236,078 |
| | | (711,499) | 5,314 |
| | | **(142,623)** | **4,974,722** |
| **Mabadiliko ya mali na dhima za uendeshaji:** | | | |
| Mabadiliko katika hifadhi ya kiwango cha chini cha kisheria | | (1,099,172) | (1,155,781) |
| Mabadiliko ya mikopo na vianzio kwa wateja | | 443,775 | (6,131,856) |
| Mabadiliko katika mali zingine | | 229,783 | (1,043,046) |
| Mabadiliko katika amana za benki | | 23,729,983 | (815,517) |
| Mabadiliko katika amana za wateja | | (1,888,073) | 16,650,075 |
| Mabadiliko katika dhima zingine | | 103,588 | (21,137) |
| Mabadiliko ya dhamana za serikali | | (16,057,937) | (12,685,923) |
| **Fedha taslimu zilizotumika katika uendeshaji** | | **5,319,324** | **(228,463)** |
| Kodi ya mapato iliyolipwa | 28 | 313,079 | (297,021) |
| **Fedha zilizotumika katika uendeshaji** | | **5,632,403** | **(525,484)** |
| **Mtiririko wa fedha katika shughuli za uwekezaji** | | | |
| Manunuzi ya mali na vifaa | 25 | (270,281) | (767,027) |
| Manunuzi ya mali zisizoshikika | 26 | (414,884) | (783,114) |
| Malipo ya haki ya matumizi ya mali zilizokodiwa | 36(ii) | - | (34,018) |
| Uwekezaji katika hisa | | 36,531 | 27,313 |
| Gawio lililopokewa | | | |
| **Fedha zilizotumika katika shughuli za uwekezaji** | | **(648,634)** | **(1,556,846)** |
| **Mtiririko wa fedha kutoka katika shughuli za kifedha** | | | |
| Gawio lililolipwa | | (15,304) | (64,748) |
| Mkopo uliyopokelewa | 31 | - | 4,000,000 |
| Malipo ya pango-Msingi | (ii)36 | (901,979) | (675,709) |
